# SHULE YA SEKONDARI GENDA

## MTIHANI MAALUM WA KUJIPIMA KIDATO CHA PILI

## KISWAHILI

**MUDA: SAA 2:30** **Julai, 2025**.

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu **A, B** na **C**.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A, B na **C** kwa wekevu na umakinifu.
3. Sehemu A ina jumla ya alama kumi na tano (15) na sehemu **B** ina jumla ya alama **sabini (70)** na sehemu **C** ina alama **15.**
4. Zingatia maelekezo ya kila swali na kila sehemu
5. Majibu yote yaandikwe kwenye nafasi za mtihani ulizopewa.
6. Vifaa vyote vya mawasiliano na visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
7. Andika namba yako ya mtihani katika kila ukurasa, sehemu ya juu upande wa kulia

## SEHEMU A (ALAMA 15)

**Jibu maswali yote katika sehemu hii**

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) hadi (x) kisha andika herufi ya jibu hilo katika karatasi ya kujibia.

 i. Mtunzi wa mashairi kutumia miundo ya aina mbalimbali ili kuipa upekee kazi yake. Upi ni muundo wa tarbia kati ya ifuatayo? (a) Mistari miwili kwa kila ubeti (b) Mistari mitatu kwa kila ubeti (c) Mistari minne kwa kila ubeti (d) Mistari mitano kwa kila ubeti

 ii. Kati ya vipengele vifuatavyo ni kipi hakihusiani na maudhui ya kazi ya fasihi? (a) Mafunzo (b) Mtazamo (c) Msimamo (d) Msisitizo

 iii. Sentensi ipi kati ya zifuatazo imeundwa kwa kuunganisha sentensi mbili? (a) Mwalimu ameingia darasani kufundisha (b) Mama alichota maji lakini yamemwagika (c) Shule yetu ya msingi ni kubwa na nzuri (d) Mvua na mawingu hutegemeana daima

 iv. Kw kawaida habari iliyofupishwa huwa na idadi ipi ya maneno kati ya haya? (a) Nusu ya maneno yote (b) Theluthi ya maneno yote (c) Robo ya maneno yote (d) Robo tatu ya maneno yote

 v. Neno lipi linadhihirisha kauli ya kutendwa katika kitenzi? (a) Pikia (b) Pikiwa (c) Pikika (d) Pikwa

 vi. Ni seti ipi inawakilisha kikamilifu muundo wa mfumo wa lugha yoyote? (a) Sauti, silabi, maneno na sentensi (b) Sauti, silabi, irabu na maneno (c) Silabi, irabu, maneno na sentensi (d) Sauti, irabu, konsonanti na maneno

 vii. Katika maneno yafuatayo ni orodha ipi yenye aina moja ya maneno? (a) Bata, nyumba, uvivu, kigoma (b) Bata, nyumba, kula, kigoma (c) Nywele, pika, andika, bata

 viii. Tamathali ya semi inayolinganisha vitu au hali mbili tofauti kwa kutumia viunganishi huitwaje? (a) Takriri (b) Sitiari (c) Tashihisi (d) Tashbiha

 ix. Jambo lipi kati ya yafuatayo ni muhimu kuzingatiwa katika uandishi wa insha? (a) Kujua jina halisi la mwandishi wa insha (b) Kujua barabra jambo linaloandikiwa insha (d) Kujua barabara mahali pa kuandikia insha

 x. Ipi ni sifa mahususi ya lugha ya mazungumzo? (a) Matumizi ya ishara (b) Matumizi ya alama (c) Matumizi ya ala (d) Matumizi ya lahaja.

| i. | ii. | iii. | iv. | v. | vi. | vii. | viii. | ix. | x. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

2. Oanisha maana ya dhana za kisarufi zilizo katika **Orodha A** na dhana husika kutoka **Orodha B**. Kisha andika jibu sahihi katika kisanduku ulichopewa.

| ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|
| i. Sehemu ya neno ambayo haibadiliki<br>ii. Umbo linalowakilisha mofimu<br>iii. Kipashio kidogo kabisa chenye maana katika neno<br>iv. Maumbo ambyo hayawezi kujitegemea yakiwa pekee<br>v. Kipashio kinachoweza kuambatanishwa kwenye mzizi wa neno na kuunda neno jipya | A. Mofu<br>B. Mofu huru<br>C. Mofimu<br>D. Kiambishi<br>E. Mofu tegemezi<br>F. Mzizi<br>G. Sarufi |

**Majibu**

| **Orodha A** | i. | ii. | iii. | iv. | v. |
|---|---|---|---|---|---|
| **Orodha B** | | | | | |

**SEHEMU B: (Alama 70)**

**Jibu maswali yote katika sehemu hii.**

3. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yote yanayofuata:

Miti ina faida nyingi sana katika maisha ya binadamu. Nchi isiyo na miti ni sawa na mtu atembeaye bila kuvaa nguo. Ipo miti ya asili na mingine ni ya kupandwa, yote hiyo ina faida lukuki kwa maisha ya binadamu.

Ongezeko la watuduniani na kutokuwa na nishati mbadala kama vile gesi na Umeme hasa sehemu za vijijini kumesababisha matumizi lufufu ya kuni na mkaa. Matumizi haya yametokana na ukosefu wa elimu ya utunzaji wa mazingira. Hali hii imesababisha jangwa kwa kuwa waswahili husema, chovya chovya humaliza buyu la asali."

Miti ina faida kadhaa katika maisha ya kiumbe yeyote duniani. Miti hutupatia hewa Safi tunayoivuta kila sekunde ya uhai wetu, kutengenezea fanicha, kutupatia matunda ili kutukinga na magonjwa na harufu ya miti ni dawa dhidi ya maadui mbalimbali kama vile nyoka.

Ukataji miti ovyo una madhara kama vile ukame, mmomonyoko wa udongo, uhaba wa hewa safi ya oksijeni na atharinyingine nyingi zinazoondoa uwepo wa viumbe hai naviumbe visivyo hai.

Kwa sasa serikali yetu imeanzisha kampeni mbalimbali za kulinda mazingira kama vile. kata mti panda mti", mti wa milenia" na "mtu mmoja miti mingi." Kampeni hizo hutolewa katika redio, runinga na vyombo vingine vya habari. Ni jukumu la kila mtu kuitunza na kuilinda misitu yetu.

**Maswali.**

a. Kutokana na habari uliyosoma
   i. Andika kichwa cha habari kwa maneno yasiyozidi matano.
   ……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………..
   ii. Unafikiri kwa nini kumekuwa na wimbi kubwa la ukataji wa miti?
   ……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………...

iii. Bainisha matumizi manne ya miti

- ……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
- ……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
- ……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
- ……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

b. Kulingana na habari uliyosoma, kampeni mbalimbali zinazotolewa katika vyombo vya habari zina umuhimu gani katika jamii?
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

c. Fupisha habari uliyosoma kwa maneno yasiyopungua 60 na yasiyozidi 70
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

4. Katika kipengele (a) –(e) bainisha dhima mbili kwa kila kiambishi kilichokolezwa wino

a. Babu a**ta**kuja kesho asubuhi

i. ……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………...

ii. ……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………...

b. Ukuta **u**meanguka

i. ……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………...

ii. ……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………...

c. Mwalimu ali**m**fundisha Bahati

i. ……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………...

ii. ……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

d. Nina**ku**penda

i. ……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

ii. ……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

e. **Si**taimba wimbo kesho

i. ……………………………………………………………………………………

ii. ……………………………………………………………………………………..

5. Bainisha shina la neno katika vitenzi vifuatavyo:
   a. Analima ……………………………………………………………………………………
   b. Alipiga ……………………………………………………………………………………..
   c. Wanacheza ………………………………………………………………………………
   d. Kilianguka …………………………………………………………………………………
   e. Atachapa……………………………………………………………………………………..

6. Fafanua makosa matano ya kisarufi kwa mifano
   a. ……………………………………………………………………………………………
      ……………………………………………………………………………………………
   b. ……………………………………………………………………………………………
      ……………………………………………………………………………………………
   c. ……………………………………………………………………………………………
      ……………………………………………………………………………………………
   d. ……………………………………………………………………………………………
      ……………………………………………………………………………………………
   e. ……………………………………………………………………………………………
      ……………………………………………………………………………………………
7. Eleza sifa tano za fasihi simulizi
   a. ……………………………………………………………………………………………
      ……………………………………………………………………………………………
   b. ……………………………………………………………………………………………
      ……………………………………………………………………………………………
      ……………………………………………………………………………………………
   c. ……………………………………………………………………………………………
      ……………………………………………………………………………………………
   d. ……………………………………………………………………………………………
      ……………………………………………………………………………………………
8. Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata:

Mada iliyo moyoni, hii ninawaletea,
Watoto wa mitaani, mada imeshafungua,
Wanapata mitihani, katika hii dunia,
Nawaonea huruma, imewatupa dunia,

Wanashinda jalalani, hayo ndiyo mazoea,
Umkute kituoni, naomba abiria,
Ni njaa mwake tumboni, ndiyo inamsumbua,
Ataomba kwa imani, huku anakulilia.

Wapo pia maaluni, vibaya wamezoea,
Hawaombi wala nini, kazi yao kukwapua,
Husimama vituni, abiria kuvizuia,
Abiria wanalia, kila kitu kimekombwa.

Twajenga taifa gani, watoto kuachilia?
Wazurure mitaani, na sisi twachekelea,
Tunadhania utani, na mwishowe tutalia,
Kwani mzaha mzaha, huutumbua usaha.

**Maswali**

a. Bainisha
   i. Muundo wa shairi ……………………………………………………………………
      ……………………………………………………………………………………........

ii. Mtindo wa shairi …………………………………………………………………………..
…………………………………………………………………………………………

b. Eleza dhamira ya mwandishi katika ubeti wa pili
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

c. Eleza kwa kifupi ujumbe wa shairi hili
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

d. Toa methali nyinge moja nyenye maana sawa na methali “Mzaha mzaha, hutumbua usaha” kama ilivyotumika katika shairi……………………………………………………….
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

e. Andika kichwa cha habari cha shairi hili kisichozidi maneno matano na kisichopungua maneno matatu………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

9. Bainisha tofauti tano zilizopo kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi
   a. ………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………
   b. ………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………
   c. ………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………
   d. ………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………
   e. ………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………

**SEHEMU C: (Alama 15)**

**Jibu swali la kumu 10).**

10. Badili barua ifuatavyo kuwa simu ya maandishi kwa kutumia maneno yasiyozidi kumu (10)

Shule ya Sekondari Busega,
S.L.P. 1010,
KASULU.
10/11/2015.

Mpendwa kaka Haruna Mashaka, kwanza shikamoo!
Habari za hapo nyumbani?. Wazazi wetu na wengine wote huko hawajambo? Mimi huku shuleni sijambo naendelea vizuri na masomo yangu.

Dhumuni la barua hii ni kukufahamisha kuwa nilipokuwa safarini kutoka nyumbani kuja shuleni, kwa bahati mbaya niliibiwa fedha za karo ya shule ulizonipa. Hivyo bado nadaiwa karo ya Shule. Tafadhali kaka nisamehe kwa usumbufu ninaokusababishia nitumie fedha zingine kwa ajili ya karo ya Shule. Kwa leo ni hayo tu.

Mdogo wako.
Neema Mashaka.
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………